**Manufaa ya Shule-chekechea kwa Mtoto Wako**

**na**

**Kuchukua Hatua ya Kusonga katika Shule ya Msingi.**

Lengo la kijitabu hiki ni kujulisha familia zinazo ishi uhamishoni Ayalandi kuhusu shule-kabla na manufaa ambazo zaweza tokea kwa watoto na wazazi wao wakati wanapo tumia hudum hizi. Huduma hizi zaweza kuitwa majina tofauti kama shule-kabla, kundi la kucheza,shule ya chekechea, Montessori na naíonra na huwa zinashughulikia watoto wa umri wa miaka 3-4. Sehemu ya pili ya kijitabu inatoa habari kwa elimu ya kiwango cha shule ya msingi katika Ayalandi kwa minajili ya kusaidia familia zilizo uhamishoni kuchukua hatua hii.

**Mwanzoni mwa Utoto**

Mwanzoni mwa utoto ni kitengo muhimu na ya kusisimua katika maisha ya mtoto, wanapo soma mengi kujisuhusu, wengine na ulimwengu unaowazunguka

Wazazi ambao wanatoa matunzo ya msingi kwa watoto wao wanasaidia watoto wao katika safari hii ya uvumbuzi na kujifunza.

Kwa watoto wengine, shule-chekechea inaweza kuwa uzoefu wa kwanza ya kuwa mbali na wazazi wao na kuwa sehemu ya kundi katka mazingira ya mafunzo yaliyo na mpangilio au yaliyopangwa.

Huduma ya shule-chekechea inatoa mikakati liyo pangwa kwa watoto wa shule-chekechea kwa jumla ya masaa yasiyozidi 3.5 kwa kila kikao. Huduma nyingi za shule-chekechea katika Ayalandi zina mikakati yaliyoundwa kwa minajili ya kucheza au mchezo wa‘ bila mpangilio’ kama inavyoitwa pia.

Utafiti unaonyesha kwamba mchezo ni hitaji muhimu kwa watoto wote na kwamba watoto ambao hawapewi nafasi ya kutosha kujieleza wenyewe kupitia kwa mchezo huenda wasikuze ujuzi unaohitajika kuafikia uwezekano kamili.

**Sehemu ya Kwanza: Manufaa ya Shule-Chekechea**

Sasa inajulikana kwamba kunaweza kuwa na manufaa mengi kwa mtoto wako katika kuhudhuria huduma bora ya shule-chekechea.

Manufaa haya yanaweza kuwa pana sana kuanzia kushughulikia hali ya maisha ya mtoto wako, kiakili, hisia, lugha na ukuzi wa maumbile. Shule-chekechea bora inaweza kuwapa watoto nafasi ya kua katika kila maeneo haya.

**Ukuzi wa Jamii**
Watot wanjifunza kuchanganyika na watoto wengine na watu wazima na jinsi ya kutaadabu katika njia ya kuheshimika na wengine. Pia wana:

- Wanafurahia na kutengeneza marafiki wapya
- Jirekebisha kuwa sehemu ya kundi kwa kugawana, kuwatunza wengine na kutatua migogoro

**Ukuzi wa Akili**
Watoto wanajifunza kutumia akili zao kukuza mawazo, kutatua shida na kujieleza wenyewe. Pia wana:

- Fanya maamuzi na kujifunza katika njia asili kupitia mchezo
- Kuza hali yao ya mafikira na ubunifu
- Kuza ujuzi wa hesabu-kabla na kusoma-kabla
- Jifunza kuhusu wao wenyewe na wengine; ulinganifu na tofauti

**Ukuzi wa Mhemuko**
Watoto wanajifunza kuhusu hisia na mhemuko. Pia wana:

- Kurekebisha kutumia wakati mbali na familia zao
- Kuza uhuru wao na ujuzi wa kujisaidia wenyewe
- Shuhudia desturi na hali ya usalama kutoka kwa haya

**Ukuzi wa Lugha**
Watoto wanajifunza kuwasiliana na wengine wakitumia maneno, misemo, vifungu vya maneno na hatimaye sentensi wakati wanakuza ujuzi wao wa lugha. Pia wana.

- Jifunza jinsi ya kusikiliza, ujuzi wa kusoma-kabla na kuandika
- Jifunza jinsi ya kutumia lugha ya ishara katika kuwasiliana
- Jifunza jinsi ya kujieleza wenyewe kwa kutumia maneno
- Jifunza Kiingereza kama lugha ya kuongezea

**Ukuzi wa Maumbile**
Watoto wanajifunza kutumia miili yao kwa njia geni wanapo kuwa na kukua. Pia wana:

- Wanapata uthibiti mkubwa sana kwa miili yao na mwondoko
- Kuza uhodari yao ya kimaumbile na afya na hali njema

Hatua ya kusonga katika shule ya msingi pia itakuwa rahisi sana kwa wazazi wote wawili na watoto wao wakiwa wanahudhuria huduma ya shule-chekechea.

Kuna manufaa mengine kwa wazazi wakati watoto wao wanapohudhuria huduma ya shule-chekechea, kama nafasi ya:

- Kutana na wengine, kuunda uhusiano na kufanya LINKS katika jumuiya ya mtaa
- Pokea msaada na habari kulingana na malezi na mada zingine
- Hudhuria kazi, mafunzo na masomo.

**Kujifunza Kiingereza kama Lugha ya Kuongezea katika Mseto wa Shule-Chekechea**

Kuna njia tofauti ambazo watoto hujifunza lugha ya kuongezea na hii inaweza kutendeka katika hatua ambazo huenda zikatendeka wakati mtoto anahudhuria shule-chekechea. Hatua hizi zinahusisha:

- Kuendelea kutumia lugha ya nyumbani kwa mtoto katika mseto wa lugha mpya
- Utumiaji wa mawasiliano ya ishara kwa mfano kukubali kwa kutingisha kichwa, kuelekeza, kutikisa kichwa, kushika na kuangaliana macho kwa macho
- Kipindi cha kimya, wakati mtoto hazungumzi kabisa – watoto wanasikiliza lugha mpya na kujenga kuelewa kwao kwa lugha
- Utumiaji wa maneno ya kurudia na misemoya maneno, na aina ya mchezo wa lugha
- Utumiaji wa maneno moja, misemo na maswali yaliyohusishwa kwa desturi ya kila siku
- Utumiaji wa sentesi ndefu na maana mwafaka, makosa huenda bado yakatokea na sarufi

Utafiti unaonyesha kwamba ni muhimu watoto wawe na nafasi ya kuendelea kukuza katika lugha zao za kwanza au za nyumbani kwani hii inasaidia kujifunza lugha ya pili.

(Kuunga mkono Utambulisho, Anuwai na Lugha katika Miaka ya Mwanzoni, 2000 Siraj-Blatchford na P.Clarke

**Kupata Shule-Chekechea**

Shule-chekechea chini ya sheria zinahitajika kujulisha Mkurugenzi wa Huduma ya Afya (HSE) kabla ya kuanzishwa. Chini ya Sheria ya utunzi wa mtoto huduma zinafaa kufuata masharti ambayo inakaguliwa na Ukaguzi wa Shule-chekechea ya HSE na Huduma ya Habari. Unaweza kuchukua orodha ya shule-chekechea ambazo zimejulishwa kwa HSE kutoka kwa Kamati yako ya Matunzo ya Watoto ya Mji wa Mtaa au Ukaguzi wa Shule ya chekechea na Huduma ya Habari. Hii itajumuisha maelezo ya mawasiliano ya huduma katika eneo lako.

Ada huenda ikatozwa kila siku, kila wiki au kiwango cha kila mwezi, hii inafaa kujadiliwa na mtumishi mshirika katika shule-chekechea.

Kuna usaidizi wa fedha unaopatikana kwa gharama ya matunzo ya mtoto. Wasiliana na shule ya chekechea ya mtaani au kamati ya Mji wa Mtaa/ Kaunti ya Matunzo ya mtoto kwa taarifa kuhusu msaada wa kifedha.

**Usalama na Ubora**

Masharti yaliyowekwa ambapo huduma za shule-chekechea ni lazima zifuate usaidizi, kuhakikisha ubora, mazingira salama kwa watoto.

Huduma za Shule-chekechea zinakaguliwa na Ukaguzi wa HSE za Shule-chekechea na Huduma za Habari na ni lazima ziafikiane na masharti ili kuendelea
**Siolta** – Mfumo wa Ubora wa Taifa kwa Elimu ya Mwanzo ya Matunzo ya mtoto na
**Aistear**, Mfumo wa Mtalaa wa Mwanzo wa Utoto ni mikakati mapya ambayo inalenga kuhakikisha kwamba watoto wote wanashuhudia huduma bora za shule-chekechea.

Mikakati hii inaipa kipaumbele umuhimu wa Usawa na Utambulisho na belong zinazoangaziwa katika matunzo ya mtoto na zinazo husishwa kwa uzito kwa **Anuwai na wa Mwongozo kwa Watoaji Matunzo ya watoto, 2006.**

**Msaada kwa Watoto katika Shule-Chekechea**

Kama mtoto wako ana ulemavu, huduma za usaidizi kama msaidizi wa mahitaji maalum huenda zikapatikana au huduma zingine huenda pia zikawa na vifaa zaidi ambazo zaweza kushughulikia mahitaji zaidi ya mtoto wako kwa mfano chumba cha ufahamu tofauti.

Wasiliana na Huduma ya Watoto ya Clare au Huduma yako ya Mtaani ya Ulemavu kwa habari ili kuulizia kuhusu wasaidizi wa huduma maalum

**Kalenda ya Shule-chekechea**

Mwaka wa shule-chekechea ikitegemea huduma inaweza kuendelea kwa wiki 38 kutoka Septemba hadi Juni na katika matukio mengine kwa mwaka mzima kwa wiki 50

## Kuchukua Hatua Kusonga katika Shule ya Msingi

**Kuanza katika Shule ya Msingi**

Umri halali wa kuanza shule ya msingi nchini Ayalandi ni miaka sita hata hivyo wazazi wengi wanachagua kuwatuma watoto wao kati ya umri wa miaka minne na tano. Watoto wanahudhuria shule ya msingi kwa miaka nane.

Kama familia yako ni geni katika Ayalandi, hata ikiwa wanatafuta hifadhi, wakimbizi au wafanyikazi walio uhamishoni, watoto wako wana haki sawa kwa elimu kama watoto waliozaliwa Ayalandi.

Elimu ya shule ya msingi nchini Ayalandi ni bure ila mtoto wako anahudhuria shule ya kibinafsi. Neno 'shule ya kitaifa' pia hutumika kuashria aina hii ya elimu.

Darasa la kwanza ambalo mtoto ataingia katika shule ya msingi inaitwa watoto wachanga, hii hufuatiwa na:

- Watoto Wakubwa
- Darasa la Kwanza
- Darasa la Pili
- Darasa la Tatu
- Darasa la Nne
- Darasa la Tano
- Darasa la Sita

Madarasa ya watoto wachanga huwa inaendeshwa kwa takriban masaa 4 hadi 4.5 kati ya saa 3 asubuhi na saa 8 mchana

Ni muhimu kuwasiliana na shule uliyochagua ili kuchukua fomu ya kusajili mtoto wako kabla ya tarehe iliyo kubaliwa ya kuanza ya mtoto wako.

**Aina ya Elimu ya Msingi**

Kuna aina tofauti ya elimu ya shule ya msingi zinazopatikana nchini Ayalandi hata hivyo kuwepo kwa shule hizi itategemea eneo. Idadi kubwa ya elimu ya shule ya msingi zinafadhiliwa na serikali na kumilikiwa na kusimamiwa na mamlaka ya kanisa kama Katoliki la Warumi na Kanisa la Ayalandi na pia kuna shule za dini tofauti ( k.m Shule ya Elimu ya Pamoja) na shule za lugha za Ayalandi (Gael Scoileanna). Hivi sasa (2010) kuna shule mbili za Kiislamu nchini Ayalandi zilizoko Dublin. Pia katika maeneo mengine kuna shule tofauti za watoto wenye ulemavu zinazoitwa Shule Maalum'.

Shule ambazo zinasimamiwa na maagizo ya kidini huwa wazi kwa watoto wanaohudhuria shule zao kutoka kwa imani zingine/dini; hatahivyo, katika maeneo mengine kipaumbele huenda ikapeanwa kwa watoto ambao dini yao ni sawa kama agizo linalosimamia shule.

Shule nyingi hutoa vikao vya habari au siku wazi kwa wazazi ili waweze kujua mengi kuhusu shule na kile ambacho inatoa kwa watoto wao.

Shule zingine itahitaji mtoto wako kuvaa sare ya shule lakini si shule zote huhitaji hii.

**Kupata Shule ya Msingi au Shule Maalum**

Idara ya Elimu na Ujuzi ina tovuti ambayo ina orodha ya shule zote za msingi katika taifa nzima. Tazama www.education.ie/home au piga simu 01 8896400

**Msaada kwa Watoto katika Shule ya Msingi**

Ikihitajika uliza shule habari kuhusu hazina zinazopatikana kwa vitabu vya shule na sare za shule.

Mtoto wako atahitajika kufanya kazi ya nyumbani wanapo hudhuria shule na shule zingine huenda zikawa na Kazi ya nyumbani au vilabu vya Baada ya Shule. Zungumza na walimu kama una shauku kuhusu njia bora za kumsaidia mtoto wako katika kukamilisha kazi zao za nyumbani na kujua kuhusu huduma zozote za misaada ambazo zinaweza kupatikana katika eneo lako.

Msaada wa kujifunza au mwalimu wa huduma za raslimali kwa kawaida hupatikana katika shule zote za msingi. Watoto wengine huenda wakawa na ugumu na mtalaa na wanahitaji masaa ya ziada ya mafunzo (ya kuongezea/zaidi). Ni mwalimu wa mafundisho ya msaada ambaye atatoa mafundisho ya ziada.

Wasaidizi wa mahitaji maalum wanaweza kusaidia katika matunzo ya wanafunzi walio na ulemavu. Wanaweza kupatikana kwa mtoto wako kwa muda maalum au muda kamili.

Kuulizia kuhusu wasaidizi wa mahitaji maalum utahitajika kuwasiliana na waandalizi wa mahitaji ya elimu maalum wa eneo lako.

Orodha ya waandalizi wa mahitaji maalum ya elimu inapatikana katika tovuti ya Baraza la Kitaifa ya Elimu Maalum WWW.NCSE.IE

**Kalenda ya Shule**

Mwaka wa shule unaanza kila Septemba na inakamilika Juni. Shule pia itafungwa kwa likizo wakati wa Krismasi, Pasaka, mapumziko ya katikati mwa muhula, likizo za benki na siku za mafunzo kwa walimu. Majengo ya shule mengine pia hutumika kwa uchaguzi wa mtaa kwa hivyo itafungwa wakati inapofanyika.

**Mawasiliano Muhimu**

- **Kamati ya Clare ya Matunzo ya Watoto ya Kaunti ya Clare,** Barabara ya 1Kilrush, Ennis, Kampuni ya. Clare. Nambari ya simu: (065) 6864862, Barua pepe: info@clarechildcare.ie Tovuti: www.clarechildcare.ie
- **Huduma ya Watoto ya Clare,** Barabara ya Lifford , Ennis, Kampuni ya .Clare. Nambari ya simu: (065) 6863500, Barua pepe: ceis@mailh.hse.ie Kamati ya Matunzo ya watoto katika Kaunti ya Clare,
- **Kundi la Msaada la Uhamiaji ya Clare,** Kitengo cha 13, CARMODY ST BUSINESS PARK

Barabara ya Carmody, Ennis, Kampuni ya. Clare, Mtu wa Kuwasiliana naye: Orla Ní Eilí, Nambari ya simu: (065) 6822026 Kipepesi: (065) 6822017, Barua pepe: cisc@eircom.net

- **Muungano wa haki za Watoto,** **Barabara ya** 4 Barabara ya, Dublin 2. Nambari ya simu: (01) 6629400, Barua pepe: info@childrensrights.ie Tovuti: www.childrensrights.ie
- **Idara ya Elimu na Ujuzi,** Afisi Kuu, Barabara ya Marlborough, Dublin 1. Nambari ya simu: (01) 8896400, Tovuti: www.education.ie/home
- **EDENN,** ( Usawa na Anuwai katika Mtandao wa Taifa ya Mwanzoni mwa Mtoto) – Wasiliana na Colette Murray 0872976823
- **Elimu ya Pamoja,** Mwakilishi wa Shirika la Shule za Elimu ya Pamoja na Mashirika yote katika Jamhuri ya Ayalandi. H8A CENTREPOINT, OAK DRIVE, Dublin 12. Nambari ya simu: (01) 429 2500, Barua pepe: info@educatetogether.ie Tovuti: www.educatetogether.ie
- **Mamlaka ya Usawa**, Barabara ya 2 ya Clonmel , Dublin 2. Nambari ya simu: LoCall 1890 245 545/ 01 4173333, Barua pepe: info@equality.ie Tovuti: www.equality.ie
- **Forbairt Naíonraí Teoranta,** 7 Cearnróg Mhuirfean, Baile Átha Cliath 2. Nambari ya simu: (01) 6398442, Barua pepe: forbairtnaionrai@eircom.net
- **Gaelscoileanna Teo,** Halla Naomh Pádraig, Institiúid Oideachais, Marino Ascaill Uí Ghríofa, Baile Átha Cliath 9. Nambari ya simu: (01) 8535195, Barua pepe: oifig@gaelscoileanna.ie Tovuti: www.gaelscoileanna.ie
- **Health Service Executive West, Pre-school Inspection and Information Services Mkurugenzi wa Huduma ya Afya WEST, Uchunguzi wa Shule-kabla na Huduma za habari,** (Afisi ya Clare Mtaani ya Afya) River House Jumba la Mto, Gort Road, Ennis, Kampuni ya Clare. Nambari ya simu: (065) 6863902, **Laini ya Habari ya Kitaifa ya HSE** 1850 241850
- **Muungano wa Chekechea ya Ayalandi Steiner,** Cappaduff, Mountshannon, Kampuni ya .Clare. Nambari ya simu: (061) 927944, Barua pepe: info@steinerireland.org Tovuti: www.steiner.org
- **Baraza la Kitaifa ya Elimu Maalum,** Barabara ya Mill , Meath. Nambari ya simu: (046) 948 6400, FAX: (046) 948 6404, Barua pepe:info@ncse.ie Tovuti: www.ncse.ie
- **Mamlaka ya Kitaifa ya Ulemavu,** Barabara ya 25 ya Cyclde, Dublin 4. nambari ya simu: (01) 6080400, Barua pepe: nda@nda.ie
- **Afisi ya Waziri wa Watoto na Mambo ya Vijana,** Jumba la Hawkins , Dublin 2. Nambari ya simu: (01) 6354000 Tovuti: www.omc.gov.ie
- **Jamii ya St. Nicholas Montessori ya Ayalandi** Jumba la Kingston , Barabara ya 64 ya Patrick , Dun Laoghaire, Co Dublin. Nambari ya simu: (01) 2805705, Barua pepe: info@montessoriireland.ie Tovuti: www.montessoriireland.ie/

Kwa orodha kamili ya mawasiliano ya **Kamati zote za Matunzo ya Watoto ya Kaunti/Mji** nenda kwa www.omc.gov.ie au piga simu 01 6345000
Kijitabu hiki kilitengenezwa na kamati ya Kaunti ya Clare ya Matunzo ya Watoto.

Tarakibu na utengenezaji wa kijitabu hiki imefadhiliwa na FÁS.

Foras Áiseanna Saothair
Training & Employment Authority

Clare County Childcare Committee
Coiste Cúram Leanaí Contae an Chláir

# Kubadilisha Ayalandi

## Imefadhiliwa na Serikali ya Ayalandi chini ya Mpango wa Ustawi wa taifa 2007-2013

NDP
National Development Plan 2007 - 2013

Office of the Minister for Children and Youth Affairs
Oifig an Aire Leanaí agus Gnóthaí Óige

pobal
government supporting communities

Swahili